**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24

**13 MACHI 2023**

## YALIYOMO


I. UTANGULIZI ..... 1
II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2022/23 ..... 3
Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2022/23 ..... 3
Sera za Mapato kwa mwaka 2022/23 ..... 3
Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 ..... 4
Mwenendo wa Mapato ..... 4
Mapato ya Ndani ..... 4
Misaada na Mikopo yenye Masharti Nafuu ..... 6
Mikopo ya Ndani yenye Masharti ya Kibiashara ..... 8
Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara ..... 8
Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali ..... 8
Mwenendo wa Matumizi ..... 9
Mafanikio Katika Utekelezaji wa Bajeti ..... 10
Changamoto Katika Utekelezaji wa Bajeti ..... 11
Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizojitokeza ..... 11
Mwelekeo wa Utekelezaji wa Bajeti Hadi Juni 2023 ..... 12
III. MAPENDEKEZO YA MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2023/24 ..... 13
Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla ..... 13
Misingi ya Uchumi Jumla (*Assumptions*): Misingi ya Bajeti ..... 13
Vihatarishi ..... 13
Sera za Mapato ..... 14
Sera za Matumizi ..... 14
Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2023/24 ..... 15
IV. MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 ..... 17
Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Katika Mafungu ..... 18
Bajeti ya Maendeleo Katika Mafungu ..... 19
V. HITIMISHO ..... 21

## I. UTANGULIZI

1. Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi; sehemu ya pili ni mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 kwa kipindi kilichoishia Januari 2023; Sehemu ya tatu ni mapendekezo ya mfumo wa bajeti ya mwaka 2023/24; sehemu ya nne ni mfumo wa bajeti kwa mwaka 2023/24; na sehemu ya tano ni hitimisho.

2. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2022/23 ni shilingi bilioni 41,480.6. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 26,474.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,006.0 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 24,122.5. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 22,236.7 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 92.2 ya lengo. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi hicho ni shilingi bilioni 23,272.5, sawa na asilimia 96.5 ya lengo, ambapo shilingi bilioni 14,635.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8,636.7 ni matumizi ya maendeleo. Matumizi zaidi ya mapato halisi ya kiasi cha shilingi bilioni 1,035.8 yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

3. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 ni pamoja na: ulipaji wa mishahara na deni la taifa kwa wakati; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kati Kwa Kiwango cha Kimataifa na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja makubwa yakiwemo Kigongo – Busisi (Mwanza) pamoja na uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba. Pamoja na mafanikio hayo, kulikuwa na changamoto kadhaa ikiwemo: Wigo mdogo wa vyanzo vya mapato, mwitikio mdogo katika ulipaji wa baadhi ya kodi, ada na tozo pamoja na baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kutumia mbinu mbalimbali kukwepa kodi; ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi ulioathiri uzalishaji wa mazao, nishati ya umeme na huduma za maji; washirika wa maendeleo kuwa na vipaumbele visivyowiana na mipango ya Serikali; na kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje hususan mafuta ya kula, bidhaa za petroli na mbolea kutokana na vita kati ya Urusi na Ukraine.

4. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa hatua hizo ni: Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuboresha huduma kwa walipa kodi, kupunguza gharama katika ulipaji wa kodi na kudhibiti upotevu wa mapato; kuendelea kutoa elimu kwa mlipakodi kuhusu manufaa ya kulipa kodi na umuhimu wa uhiari wa kulipa kodi; kuwezesha mafungu na kufuatilia kwa karibu utendaji wa Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba ya ufanisi na Maafisa Masuuli katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli; kuendelea kujenga mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo ili kuongeza wigo wa kupata misaada na mikopo nafuu; kutekeleza Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2021 na mkakati wake pamoja na kuchimba visima virefu na mabwawa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu (domestic use) na kiuchumi

kama umwagiliaji na ufugaji;  na kutoa ruzuku kwa baadhi ya bidhaa ili kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei.

5. Mapendekezo ya mfumo na ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 yameandaliwa kwa kuzingatia mwenendo halisi wa utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha hadi Januari 2023, hususan katika mwenendo wa upatikanaji wa mapato kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje pamoja na: ugharamiaji halisi wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115 ujenzi wa reli ya kati ya kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway- SGR); ulipaji wa mishahara; ulipaji wa Deni la Serikali; na matumizi mengine muhimu ya Serikali.

6. Bajeti ya mwaka 2023/24 ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 utajumuisha ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Mwaka 2023/24, jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 zinatarajiwa kukusanywa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 31,381.0 zitatokana na mapato ya ndani, shilingi bilioni 5,466.2 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shilingi bilioni 7,540.8 ni mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara. Matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 44,388.1 ambapo shilingi bilioni 29,232.1 zitakuwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,156.0 matumizi ya maendeleo.

## II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2022/23

### Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2022/23

7. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2022/23 ni shilingi bilioni 41,480.6 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 26,474.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,006.0 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

### Jedwali Na. 1: Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2022/23

(Shilingi milioni)

| ***Bajeti ya mwaka 2022/23*** | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **Vyanzo vya Mapato** | | **Matumizi** | |
| | | Matumizi ya Kawaida | |
| Mapato ya ndani | 27,005,581 | Mishahara | 9,830,753 |
| Mapato ya Halmashauri | 1,012,286 | | |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1,949,480 | Matumizi mengine | 5,335,461 |
| Mikopo ya Ndani (Miradi ya Maendeleo) | 2,480,148 | **Mfuko Mkuu (CFS)** | |
| Mikopo ya Ndani (Rollover) | 3,300,000 | Riba | 2,870,961 |
| Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara | 3,034,004 | Madeni (Principal) | 6,216,041 |
| | | Mengineyo | 2,221,362 |
| | | | |
| **Jumla ndogo** | **38,781,499** | **Jumla ndogo** | **26,474,578** |
| | | | |
| Miradi ya maendeleo (Nje) | **2,699,081** | Matumizi ya Maendeleo | **15,006,002** |
| Misaada/Mikopo ya Basket | 122,123 | Fedha za ndani | 12,306,921 |
| Misaada/Mikopo ya Miradi | 2,576,958 | Fedha za nje | 2,699,081 |
| | | | |
| **Jumla Kuu** | **41,480,580** | **Jumla Kuu** | **41,480,580** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango*

### Sera za Mapato kwa mwaka 2022/23

8. Katika mwaka 2022/23 Serikali imeendelea kuweka vipaumbele zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero;

(ii) Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na kuongeza wigo wa kodi;

(iii) Kutanua wigo wa mapato;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato;

(v) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato; na

(vi) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa na kuzuia matumizi mabaya ya misamaha.

### Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023

9. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 24,122.5. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 22,236.7 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 92.2 ya lengo. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi hicho ni shilingi bilioni 23,272.5, sawa na asilimia 96.5 ya lengo, ambapo shilingi bilioni 14,635.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 8,636.7 ni matumizi ya maendeleo. Matumizi zaidi ya mapato halisi ya kiasi cha shilingi bilioni 1,035.8 yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

### Mwenendo wa Mapato

### Mapato ya Ndani

10. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 15,625.3, sawa na asilimia 97.1 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 16,084.9. Kati ya mapato hayo: mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi bilioni 13,601.2, sawa na asilimia 98.8 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 13,763.8; mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,461.4, sawa na asilimia 84.6 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,728.2; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 562.6 ikiwa ni asilimia 94.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 592.8. **Jedwali Na. 2** linaonesha mchanganuo wa mapato ya ndani.

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani kwa Julai hadi Januari 2023**

(Shilingi milioni)

| | Aina ya Mapato | Bajeti 2022/23 | Julai 2022 - Januari 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Makadirio | Mapato Halisi | Ufanisi |
| **A.** | **Mapato yanayokusanywa na TRA (Mapato Halisi)** | **23,652.8** | **13,763.8** | **13,601.2** | **98.8%** |
| | Toa Marejesho ya Kodi | **-657.8** | **-399.3** | **-642.2** | **160.8%** |
| | **Jumla Ndogo (Mapato Ghafi)** | **24,310.6** | **14,163.1** | **14,243.4** | **100.6%** |
| 1 | Ushuru wa Forodha | 1,579.3 | 927.2 | 994.6 | **107.3%** |
| 2 | Ushuru wa Bidhaa -Nje | 1,628.5 | 956.1 | 806.8 | **84.4%** |
| 3 | Ushuru wa Bidhaa-Ndani | 1,574.8 | 938.1 | 945.4 | **100.8%** |
| 4 | Kodi ya Ongezeko la Thamani-Nje | 3,581.7 | 2,102.9 | 2,172.1 | **103.3%** |
| 5 | Kodi ya Ongezeko la Thamani-Ndani | 3,742.6 | 2,154.7 | 2,138.2 | **99.2%** |
| 6 | Kodi ya Mapato | 7,871.5 | 4,442.7 | 4,456.0 | **100.3%** |
| 9 | Mapato yasiyo ya kodi | 1,252.3 | 827.6 | 791.4 | **95.6%** |
| 10 | Kodi nyingine | 3,079.9 | 1,813.9 | 1,938.9 | **106.9%** |
| **B.** | **Mapato yasiyo ya kodi** | **3,352.8** | **1,728.2** | **1,461.4** | **84.6%** |
| 11 | Michango na Gawio ya Mashirika | 933.0 | 376.9 | 485.7 | **128.9%** |
| 12 | Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa | 2,419.8 | 1,351.4 | 975.7 | **72.2%** |
| | **Jumla ya Mapato (A+B)** | **27,005.6** | **15,492.1** | **15,062.7** | **97.2%** |
| **C.** | **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | **1,012.3** | **592.8** | **562.6** | **94.9%** |
| | | | | | |
| | **Jumla ya Mapato ya Ndani (A+B+C)** | **28,017.9** | **16,084.9** | **15,625.3** | **97.1%** |

***Chanzo****: Wizara ya Fedha na Mipango*

**Mchanganuo wa Mapato Yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA**

11. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (ya kodi na yasiyo ya kodi) yalifikia shilingi bilioni 13,601.2, sawa na asilimia 98.8 ya lengo la shilingi bilioni 13,763.8 katika kipindi hicho. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 12,809.8 na mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 791.4. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 642.2 zilitumika kulipa marejesho mbalimbali ya kodi (Tax refund) ambapo kati ya marejesho hayo, shilingi bilioni 524.9 ni marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kutofikiwa kwa lengo kulitokana na baadhi ya wafanyabiashara wasiokua waaminifu kuendelea kutumia mbinu mbalimbali kukwepa kodi.

12. Katika kipindi kilichobaki hadi Juni 2023, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa kodi ili kufikia malengo, zikiwemo zifuatazo:

(i) Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka yote nchini kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo;
(ii) Kuendelea kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA (EFDMS, TANCIS, ITAX) kwa ajili ya kufatilia kiasi cha fedha kinachopaswa kulipwa na walipakodi;
(iii) Kushirikisha Taasisi za Serikali katika kusaidia urejeghaji wa madeni ya kodi kutoka kwa wauzaji wa bidhaa na huduma kwa taasisi za umma;
(iv) Kuendelea na kampeni mbalimbali nchini za kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari kwa lengo la kupata maoni juu ya njia bora ya kuwahudumia ili kuongeza uhiari wa kulipa kodi ;
(v) Kuendelea na utaratibu wa kuingia makubaliano na walipakodi ili kuwawezesha kulipa madeni yao kwa awamu; na
(vi) Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zenye lengo la kupanua wigo wa kodi hasa katika maeneo ya biashara mtandao na wachimbaji wadogo wa madini.

**Mchanganuo wa Mapato Yasiyo ya Kodi**

13. Mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, yalifikia shilingi bilioni 1,461.4 ikiwa ni asilimia 84.6 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,728.2. Kati ya makusanyo hayo, shilingi bilioni 975.7 zilitoka kwa Wizara na Idara Zinazojitegemea na shilingi bilioni 485.7 ni mapato yatokanayo na michango na gawio kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma. Kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kulitokana na changamoto mbalimbali ikiwemo mwitikio mdogo wa wamiliki wa ardhi kulipa ada na tozo za ardhi kwa wakati. **Jedwali Na. 3** linaonesha mchanganuo wa mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara na Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma.

14. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka kwenye mafungu zikiwemo: kuwezesha mafungu na kufuatilia kwa karibu utendaji wa Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba ya ufanisi na Maafisa Masuuli katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato; kuendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuhimiza matumizi ya mfumo huo ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali; kuendelea kufanya ufuatiliaji wa vyanzo

vinavyokusanya mapato yasiyo ya kodi; na kuendelea kuimarisha mifumo ya Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati.

**Jedwali Na. 3: Makusanyo ya Mapato yasiyo ya Kodi kwa Kipindi cha Julai hadi Januari 2023** (Shilingi milioni)

| TAARIFA YA MAPATO YASIYO YA KODI YANAYOKUSANYWA NA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti 2022/23** | **Julai 2022 - Januari 2023** | | |
| | | | **Makadirio** | **Mapato Halisi** | **Ufanisi %** |
| 5 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 126,100.0 | 58,846.7 | 394.5 | 0.7 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 933,029.3 | 376,856.7 | 485,728.1 | 128.9 |
| 14 | Wizara ya Mambo ya Ndani-Jeshi la Zimamoto na | 11,000.0 | 6,416.7 | 6,127.7 | 95.5 |
| 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 60,100.0 | 1,087.2 | 1,188.1 | 109.3 |
| 28 | Wizara ya Mambo ya Ndani-Jeshi la Polisi | 94,500.0 | 55,958.9 | 52,455.6 | 93.7 |
| 29 | Wizara ya Mambo ya Nchi- Jeshi la Magereza | 1,500.0 | 857.0 | 232.5 | 27.1 |
| 34 | Afrika Mashariki | 1,559.9 | 960.9 | 461.7 | 48.0 |
| 37 | Serikali | 6,000.0 | 3,500.0 | 826.8 | 23.6 |
| 40 | Mfuko wa Mahakama | 12,571.2 | 7,333.2 | 5,238.1 | 71.4 |
| 43 | Wizara ya Kilimo | 5,017.7 | 2,927.0 | 3,005.0 | 102.7 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 900.0 | 573.6 | 419.8 | 73.2 |
| 46 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 240,100.0 | 140,058.3 | 105,174.7 | 75.1 |
| 48 | Makazi | 250,100.0 | 143,975.0 | 103,594.9 | 72.0 |
| 49 | Wizara ya Maji | 1,200.0 | 700.0 | 676.8 | 96.7 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 1,000.0 | 583.3 | 210.0 | 36.0 |
| 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 500.0 | 250.0 | 276.5 | 110.6 |
| 52 | Wizara ya Afya | 230,000.0 | 134,481.6 | 90,690.7 | 67.4 |
| 53 | Wanawake na Makundi Maalum | 8,500.0 | 5,026.0 | 2,533.1 | 50.4 |
| 64 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Uvuvi | 40,000.0 | 23,202.2 | 12,266.9 | 52.9 |
| 65 | Ulemavu | 45,000.0 | 26,250.0 | 18,724.6 | 71.3 |
| 68 | Habari | 150,700.0 | 78,466.5 | 22,815.6 | 29.1 |
| 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 9,507.4 | 5,243.2 | 6,668.5 | 127.2 |
| 93 | Uhamiaji | 260,100.0 | 149,687.6 | 116,103.8 | 77.6 |
| 96 | Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo | 900.0 | 525.0 | 524.6 | 99.9 |
| 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Mifugo | 40,100.0 | 23,391.7 | 15,122.2 | 64.6 |
| 100 | Wizara ya Madini | 822,028.2 | 480,597.0 | 409,530.6 | 85.2 |
| | Wizara nyingine na Mikoa | 810.2 | 472.6 | 444.7 | 94.1 |
| | **Jumla** | **3,352,823.8** | **1,728,227.8** | **1,461,436.2** | **84.6** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

### Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa

15. Mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 562.6 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, sawa na asilimia 94.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 592.8.

### Misaada na Mikopo yenye Masharti Nafuu

16. Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23 shilingi bilioni 4,648.6 ikijumuisha misaada shilingi bilioni 979.4, na mikopo nafuu shilingi bilioni 3,669.2. Aidha, kati ya fedha zilizoahidiwa: misaada na mikopo ya

kibajeti ni shilingi bilioni 1,949.5; mifuko ya pamoja ya kisekta ni shilingi bilioni 122.1; na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 2,577.0.

17. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2022/23, shilingi bilioni 3,087.4 zimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 90.6 ya lengo la shilingi bilioni 3,407.1. Kutofikiwa kwa lengo kunatokana na kubadilika kwa sera za ufadhili za misaada za Washirika wa Maendeleo kwa Nchi zinazoendelea, pamoja na athari ya vita kati ya Urusi naUkraine ambayo imesababisha nchi za Ulaya kupunguza fedha za misaada. Kati ya kiasi kilichotolewa, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (GBS) ilikuwa shilingi bilioni 1,498.5, sawa na asilimia 91.5 ya lengo, misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta ni shilingi bilioni 64.1, sawa na asilimia 58.6 ya lengo, na misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,524.7, sawa na asilimia 91.8. ya lengo la kipindi cha marejeo. Kupungua kwa fedha za misaada na mikopo nafuu ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta kutokana na Washirika wa Maendeleo kutopendelea muundo huu ikilinganishwa na muundo wa miradi ya maendeleo ambao ufanisi wa utekelezaji wake unapimika moja kwa moja. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Misaada na Mikopo Nafuu kwa Julai 2022 hadi Januari 2023**

(Shilingi milioni)

| Miundo wa Ufadhili | Aina ya Ufadhili | Bajeti 2022/23 | Makadirio (Julai 2022 - Januari 2023) | (Julai 2022 - Januari 2023) | Ufanisi |
|---|---|---|---|---|---|
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | Misaada | 55,530.4 | - | - | - |
| | Mikopo Nafuu | 1,893,949.4 | 1,636,959.5 | 1,498,511.7 | 91.5% |
| **Jumla Ndogo** | | **1,949,479.8** | **1,636,959.5** | **1,498,511.7** | **91.5%** |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | Misaada | 122,122.8 | 109,458.4 | 64,104.8 | **58.6%** |
| | Mikopo Nafuu | - | - | - | 0.0% |
| **Jumla Ndogo** | | **122,122.8** | **109,458.4** | **64,104.8** | **58.6%** |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | Misaada | 923,835.7 | 623,954.6 | 333,119.0 | **53.4%** |
| | Mikopo Nafuu | 1,668,122.3 | 1,036,763.2 | 1,191,621.50 | **114.9%** |
| **Jumla Ndogo** | | **2,591,958.0** | **1,660,717.8** | **1,524,740.5** | **91.8%** |
| **Jumla Kuu** | | **4,663,560.7** | **3,407,135.7** | **3,087,357.0** | **90.6%** |

***Chanzo***: *Wizara ya Fedha na Mipango*

18. Serikali inaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa ufanisi kulingana na mpango kazi uliokubalika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Hii itawezesha fedha zilizoahidiwa kutolewa kwa wakati na hivyo kutoathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, Serikali imepanga kuboresha mfumo wa D-Fund MIS kwa kuunganisha na Mifumo ya Fedha ya Benki za Biashara ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa za fedha za miradi zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo kwa wakati.

19. Serikali inaendelea kuimarisha na kuratibu juhudi za pamoja na Washirika wa Maendeleo za upatikanaji wa rasilimali fedha na uwekezaji kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF).

**Mikopo ya Ndani yenye Masharti ya Kibiashara**

20. Katika mwaka 2022/23, Serikali ilipanga kukopa katika soko la ndani kiasi cha shilingi bilioni 5,780.1. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,480.1 ni mikopo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa bajeti na shilingi bilioni 3,300.0 ni mikopo kwa ajili ya kulipia hatifungani zilizoiva. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2022/23, Serikali imefanikiwa kukopa shilingi bilioni 2,971.9, sawa na asilimia 91.2 ya kiasi kilichopangwa kukopwa cha shilingi bilioni 3,260.0 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichokopwa, shilingi bilioni 2,117.0 zilitumika kulipia hatifungani zilizoiva na shilingi bilioni 854.9 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa kiasi kilichopangwa kukopwa katika soko la ndani kinapatikana bila kuathiri ukopaji wa sekta binafsi. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu zaidi kwa wananchi na wadau wengine ili waweze kuwekeza katika dhamana za Serikali.

**Mikopo ya Nje yenye Masharti ya Kibiashara**

21. Katika mwaka 2022/23, Serikali ilipanga kukopa kiasi cha shilingi bilioni 3,034.0 kutoka vyanzo vyenye masharti ya kibiashara. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, Serikali imefanikiwa kukopa shilingi bilioni 552.3 kutoka benki za nje ya nchi ikiwa ni sawa na asilimia 40.3 ya kiasi cha shilingi bilioni 1,370.9 kilichopangwa kukopwa kwa kipindi hicho. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za kupata mkopo wenye thamani ya shilingi bilioni 1,234.0 (euro milioni 500) kutoka benki ya Deutsche. Vilevile, Serikali inaendelea kukamilisha ukopaji wa kiasi cha shilingi bilioni 1,169.0 (dola za Marekani milioni 500) ili kukamilisha lengo la mwaka.

**Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali**

22. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba, 2022 imeonesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo inaonesha kuwa mwaka 2021/22: Thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 32.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 18.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 120 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180. Aidha, uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ni asilimia 13.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15. **Jedwali Na. 5** linaonesha tathmini ya uhimilivu wa deni.

23. Katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:

(i) Kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu kadri

inavyopatikana. Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi;

(ii) Kuboresha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali; na

(iii) Kuendelea kutokutoa dhamana ya Serikali kwa taasisi za umma zinazojiendesha kwa kutegemea ruzuku. Hii itasaidia kutokuongeza deni linalotokana na taasisi zinazoshindwa kulipa madeni.

**Jedwali Na. 5: Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (Asilimia)**

| Viashiria Vya Uhimilivu | Ukomo | 21/22 | 22/23 | 23/24 | 24/25 | 25/26 | 26/27 | 27/28 | 32/33 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Deni la Nje** | | | | | | | | | |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Pato la Taifa | **40** | 18.1 | 17.7 | 17.3 | 16.4 | 15.8 | 15.8 | 16.3 | 15.4 |
| Uwiano wa thamani ya sasa ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | **180** | 119.6 | 113.4 | 108.1 | 104.0 | 101.9 | 101.3 | 99.7 | 92.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi | **15** | 13.5 | 14.1 | 9.6 | 8.9 | 8.5 | 8.2 | 8.8 | 10.6 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **18** | 14.1 | 14.9 | 10.4 | 9.6 | 9.3 | 9.3 | 10.9 | 12.2 |
| **Deni la Serikali (Ndani na Nje)** | | | | | | | | | |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa pato la Taifa | **55** | 32.5 | 31.9 | 30.9 | 29.5 | 28.4 | 27.8 | 28.6 | 30.8 |
| Uwiano wa Thamani ya sasa ya Deni kwa Mapato | **N/A** | 217 | 207 | 202 | 196 | 194 | 195 | 207.7 | 207.1 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | **N/A** | 34.0 | 41.6 | 33.3 | 30.5 | 27.6 | 27.7 | 30.1 | 41.0 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Mwenendo wa Matumizi**

24. Sera za Matumizi katika mwaka 2022/23 zinajumuisha yafuatayo: Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya; Kutenga fedha na kulipa madeni yaliyohakikiwa na kudhibiti uzalishaji wa madeni mapya na ulimbikizaji wa madeni; kuboresha mishahara ya watumishi wa umma na kugharamia Deni la Serikali kwa kutumia mapato ya ndani; kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya asili na athari za magonjwa ya mlipuko ikiwa ni pamoja na UVIKO – 19; kuendelea kujenga mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi; kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kudhibiti matumizi ya Serikali na kujenga uwezo wa wataalam wa ndani katika eneo la

ulinzi na usalama wa mifumo (systems security) inayodhibiti matumizi; na kugharamia Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

**Matumizi ya Serikali**

25. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi kilichoishia Januari, 2023 ilikuwa shilingi bilioni 23,272.5, sawa na asilimia 96.5 ya lengo. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 14,635.8 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 95.7 ya lengo na shilingi bilioni 8,636.7 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 97.8. Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 5,226.3 kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 5,212.8 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na shilingi bilioni 4,196.7 kwa ajili matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 7,047.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 1,588.9 fedha za nje. Mchanganuo wa utoaji wa ridhaa ya matumizi kwa kipindi cha Julai hadi Januari 2022/23 ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Mchanganuo wa utoaji wa ridhaa ya matumizi kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023**

(Shilingi bilioni)

| MATUMIZI | Bajeti ya Mwaka 2022/23 | Makadirio (Jul,22 - Jan,23) | Halisi (Jul,22 - Jan,23) | UFANISI |
|---|---|---|---|---|
| | Shilingi bilioni | | | |
| Deni la Serikali | 9094.0 | 5252.2 | 5212.8 | 99.3% |
| Mishahara (PE) | 9830.8 | 5587.1 | 5226.3 | 93.5% |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 7549.8 | 4454.3 | 4196.7 | 94.2% |
| Maendeleo - Ndani | 12306.9 | 7179.0 | 7047.9 | 98.2% |
| Maendeleo - Nje | 2699.1 | 1650.0 | 1588.9 | 96.3% |
| **Jumla** | **41,480.6** | **24,122.5** | **23,272.5** | **96.5%** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango

**Mafanikio Katika Utekelezaji wa Bajeti**

26. Mafanikio mengine katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Januari 2023 yanajumuisha;

(i) Kuwezesha upatikanaji wa fedha za kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali kwa asilimia 96.5 ikilinganishwa na asilimia 95.5 ya kipindi kama hicho mwaka 2021/22;

(ii) Utoaji wa ruzuku kwenye bidhaa za mafuta nchini kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kuleta nafuu kwa watumiaji ambapo jumla ya shilingi bilioni 477.1 zimetumika;

(iii) Utoaji wa ruzuku kwenye mbolea kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza gharama kwa mkulima ambapo jumla ya tani 297,599.18 za mbolea zimesambazwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa bei ya punguzo ya wastani wa shilingi 70,000 kwa mfuko ikilinganishwa na wastani wa bei ya soko ya shilingi 140,000. Jumla ya shilingi bilioni 222.5 zimetumika;

(iv) Kukamilika kwa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambapo jumla ya shilingi bilioni 117.81 zilitumika mwaka 2021/22 na shilingi bilioni 302.59 zilitumika mwaka 2022/23;

(v) Kukua kwa sekta ya utalii kutokana na na juhudi za kutangaza utalii ikiwemo *Royal Tour*;

(vi) Kuimarika kwa uhifadhi, ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu; kukua kwa demokrasia na hakijinai

(vii) Kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kukusanyia mapato ambayo imepunguza uvujaji wa mapato katika baadhi ya maeneo yanayosimamiwa na TRA, MDAs na LGAs; na

(viii) Kuongezeka kwa ufanisi wa kukusanya mapato ya kodi, ambapo ukuaji ulifikia asilimia 11.1 kwa kipindi cha Julai hadi Januari 2022/23 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilivunja rekodi ya ukusanyaji wa kodi mwezi Disemba 2022 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2,765.5 kilipatikana ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kukusanywa, sawa na asilimia 106.5 ya lengo na ukuaji wa asilimia 10.3.

**Changamoto Katika Utekelezaji wa Bajeti**

27. Pamoja na mafanikio hayo, zipo changamoto zilijitokeza ambazo Serikali inaendelea kukabiliana nazo zikiwemo:

(i) Wigo mdogo wa vyanzo vya mapato, mwitikio mdogo katika ulipaji wa baadhi ya kodi, ada na tozo pamoja na baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kutumia mbinu mbalimbali kukwepa kodi;

(ii) Ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi ulioathiri uzalishaji wa mazao, nishati ya umeme na huduma za maji;

(iii) Washirika wa maendeleo kuwa na vipaumbele visivyowiana na mipango ya Serikali; na

(iv) Kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje hususan mafuta ya kula, bidhaa za petroli na mbolea kutokana na vita kati ya Urusi na Ukraine.

**Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Zilizojitokeza**

28. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuchachua uchumi, kuongeza mauzo nje na mapato ya Serikali na kuimarisha usimamizi wa matumizi ili kufikia malengo katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2022/23. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na:

(i) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kuboresha huduma kwa walipa kodi, kupunguza gharama katika ulipaji wa kodi na kudhibiti upotevu wa mapato ikiwa ni pamoja na kuhuisha kanzidata ya wamiliki wa ardhi ili kuendana na mfumo wa bili (billing system);

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari kuhusu manufaa ya kulipa kodi na umuhimu wa uhiari wa kulipa kodi;

(iii) Kuwezesha mafungu na kufuatilia kwa karibu utendaji wa Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba ya ufanisi na Maafisa Masuuli katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli;

(iv) Kuendelea kujenga mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo ili kuongeza wigo wa kupata misaada na mikopo nafuu;

(v) Kutekeleza Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira

wa mwaka 2021 na mkakati wake pamoja na kuchimba visima virefu na mabwawa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu (domestic use) na kiuchumi kama umwagiliaji na ufugaji; na

(vi) Kutoa ruzuku kwa baadhi ya bidhaa ili kupunguza kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei.

**Mwelekeo wa Utekelezaji wa Bajeti Hadi Juni 2023**

29. Mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato utalenga katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki, kudhibiti uvujaji wa mapato na kuimarisha kaguzi za kodi. Aidha, Serikali itaendelea kudhibiti matumizi ili kuendana na mpango na bajeti.

30. Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha zinaelekezwa kama zilivyoidhinishwa kwenye maeneo yenye tija kwa taifa. Aidha, Serikali itajielekeza zaidi katika kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji ikiwemo kupunguza urasimu, maboresho ya sheria, kanuni, taratibu za uratibu, sera, kuweka vivutio vya kodi na ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, bandari, nishati).

31. Kwa kipindi kilichobaki (Februari hadi Juni 2023), utekelezaji wa bajeti ya Serikali utahitaji jumla ya shilingi bilioni 18,208.1 kutoka vyanzo vyote vya mapato. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 6,369.3 zinatarajiwa kuelekezwa katika matumizi ya maendeleo na shilingi bilioni 11,838.8 katika matumizi ya kawaida. **Jedwali Na. 7** linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 na mwelekeo hadi Juni 2023.

**Jedwali Na. 7: Mfumo wa Bajeti wa mwaka 2022/23 na Mwelekeo hadi Juni 2023**

| | | | | | Shilingi Bilioni |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Bajeti ya Mwaka 2022/23** | **Makadirio (Jul,22 - Jan,23)** | **Halisi (Jul,22 - Jan,23)** | **Ufanisi (Jul,22 - Jan,23)** | **Makadirio (Feb - Jun, 23)** |
| | **Shilingi bilioni** | | | | **Shilingi bilioni** |
| **Mapato ya Ndani** | **28,017.87** | **16,084.5** | **15,625.3** | **97.1%** | **12,392.57** |
| Mapato ya TRA | 23,652.8 | 13,763.8 | 13,601.2 | 98.8% | 10,051.53 |
| Mapato yasiyo ya Kodi | 3,352.8 | 1,727.8 | 1,461.4 | 84.6% | 1,891.39 |
| Mapato ya Halmashauri | 1,012.3 | 592.8 | 562.6 | 94.9% | 449.66 |
| Misaada na Mikopo Nafuu | 4,648.6 | 3,407.1 | 3,087.4 | 90.6% | 1,561.20 |
| Mikopo ya Kibiashara nje | 3,034.0 | 1,370.9 | 552.2 | 40.3% | 2,481.80 |
| Mikopo ya Ndani | 5,780.1 | 3,260.0 | 2,971.9 | 91.2% | 2,808.29 |
| Mkopo wa muda mfupi (BOT) | | | 1,035.8 | | (1,035.79) |
| **Jumla ya Mapato Yote** | **41,480.6** | **24,122.5** | **23,272.5** | **96.5%** | **18,208.08** |
| | | | | | |
| **Jumla ya Matumizi Yote** | **41,480.6** | **24,122.5** | **23,272.5** | **96.5%** | **18,208.08** |
| Mishahara | 9,830.75 | 5,587.05 | 5,226.3 | 93.5% | 4,604.47 |
| Deni la Serikali | 9,093.98 | 5,252.16 | 5,212.8 | 99.3% | 3,881.17 |
| Matumizi Mengineyo | 7,549.84 | 4,454.29 | 4,196.7 | 94.2% | 3,353.14 |
| **Maendeleo Jumla** | **15,006.0** | **8,829.0** | **8,636.7** | **97.8%** | **6,369.29** |
| Maendeleo Ndani | 12,306.92 | 7,179 | 7,047.9 | 98.2% | 5,259.07 |
| Maendeleo Nje | 2,699.08 | 1,650 | 1,588.9 | 96% | 1,110.22 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

## III. MAPENDEKEZO YA MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2023/24

### Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla

32. Shabaha na malengo ya uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 7.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23 kutoka matarajio ya asilimia 11.5 mwaka 2022/23;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### Misingi ya Uchumi Jumla (*Assumptions*): Misingi ya Bajeti

33. Uandaaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 umezingatia misingi (*assumptions*) ifuatayo:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(iii) Kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

### Vihatarishi

34. Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali ikiwemo: Mfumuko wa bei; viwango vya kubadilisha fedha; ukuaji wa Pato la Taifa; viwango vya riba katika soko la fedha la ndani na nje; mabadiliko ya tabianchi (ukame/mafuriko) na uharibifu wa mazingira; majanga asilia kama vile matetemeko ya ardhi na magonjwa ya mlipuko; mabadiliko ya sera za ufadhili za misaada za Washirika wa Maendeleo kwa nchi zinazoendelea; ubadhirifu wa fedha na mali za umma; na madeni sanjari (contingent liabilities).

35. Athari zinazoweza kujitokeza endapo vihatarishi vya mwenendo wa uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti vitatokea ni pamoja na: kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato; kupungua kwa uzalishaji viwandani na mashambani; kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za maisha

kwa wananchi na utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali; kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha; kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma; na kuongezeka kwa Deni la Serikali.

36. Ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali itaendelea na mikakati na hatua za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na: kusimamia miongozo ya kubaini vihatarishi katika uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ili kuchukua hatua stahiki za kisera na kiutawala kabla, wakati na baada ya kutokea; kuimarisha uwezo wa Serikali katika kupambana na vitendo vya ukwepaji kodi ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa biashara za magendo, utoaji wa elimu kwa mlipakodi pamoja na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato; kutoa unafuu wa upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbolea, zana za kilimo, viuatilifu, mbegu bora na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Katika kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbolea nchini, Serikali inaendelea kutoa ruzuku ya mbolea na kuvipa kipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea katika matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji. Mikakati mingine ni: kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali; kusimamia sera za fedha na bajeti kwa weledi ili kufikia malengo na shabaha za kiuchumi ikiwemo kudhibiti mzunguko wa fedha kulingana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi; kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi na taasisi zote za umma ili kuwezesha maamuzi ya kiutendaji kufanyika kwa wakati; uimarisha ukaguzi wa papo kwa papo (real time audit) ili kuipa taasisi uwezo wa kubaini changamoto katika utekelezaji mapema na kuchukua hatua stahiki kupunguza athari hasi katika utekelezaji wa mpango na bajeti; na kuendelea kusimamia Deni la Serikali kwa weledi.

**Sera za Mapato**

37. Sera na mikakati ya mapato ya ndani katika mwaka 2023/24 zinalenga kuongeza makusanyo kwa kutekeleza hatua zifuatazo:

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini katika sekta za uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;
(ii) kuongeza wigo wa mapato;
(iii) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;
(iv) Kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuongeza uwekezaji ili kuongeza mapato;
(v) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa;
(vi) Kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuibua fursa mpya za mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; na
(vii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu kwa wakati.

**Sera za Matumizi**

38. Katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya

fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Lengo kuu ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, na kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikijumuisha mishahara na deni la taifa. Aidha, Serikali itaendelea kugharamia matumizi ya maendeleo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa Taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji na Wakala wa Maji Vijijini. Vilevile, Serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai pamoja na kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na unaoendana na ubora na thamani ya fedha katika ununuzi wa umma.

39. Mikakati ya kusimamia matumizi inalenga kuongeza tija na ufanisi pamoja na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo;
(ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo yenye kukuza uchumi, kuongeza mauzo nje na kuongeza mapato ya Serikali;
(iii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele ikiwemo sekta za uzalishaji (kilimo, mifugo, uvuvi, madini) hususan kwenye kuongeza thamani ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanza miradi mipya;
(iv) Kuendelea kusimamia Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni pamoja na kutenga bajeti na kulipa madeni yaliyohakikiwa;
(v) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika serikalini ili kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali;
(vi) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kuendesha vikao kwa njia ya mtandao (virtual meetings) na kuepuka matumizi ya makaratasi;
(vii) Kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwa wakati ili kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi; na
(viii) Kudhibiti matumizi ya Serikali kwenye eneo la ununuzi, uendeshaji na matengenezo ya magari.

**Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2023/24**

40. Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2023/24 yatakuwa ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Maeneo ya vipaumbele yatakayozingatiwa ni kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya

mwaka 2023/24 utajumuisha ugharamia wa: miradi ya kielelezo inayoendelea; deni la Serikali; mishahara ya watumishi wa Umma; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025; na huduma za jamii zikiwemo afya, elimu, maji na kuimarisha misingi ya usawa mbele ya sheria. Aidha, Serikali itaweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji ambazo zina fursa za kukuza uchumi, kuongeza mauzo nje, kupunguza utegemezi wa bidhaa toka nje na kuongeza mapato ya Serikali; kutekeleza diplomasia ya uchumi; kuimarisha mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa buluu.

## IV. MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

41. Kwa kuzingatia sera za bajeti kwa mwaka 2023/24, Mfumo wa Bajeti unaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 7.0 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/23 ya shilingi bilioni 41,480.6. Mapendekezo ya Mfumo wa Ukomo wa bajeti kwa mwaka 2023/24 yameongezeka ikilinganishwa na makadirio ya awali yaliyowasilishwa kwenye Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 kutokana na kumalizika kwa mazungumzo na Benki ya Dunia pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika ambao wameahidi kutoa shilingi bilioni 1,166.9 na shilingi bilioni 247.4, mtawalia. Mfumo huu wa bajeti pia umezingatia makubaliano baina ya Serikali na Shirika la Fedha la Kimataifa chini ya programu ya *Extended Credit Facility* (ECF). Makubaliano hayo yanajumuisha: Kuhakikisha kuwa uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa unaongezeka mwaka hadi mwaka; kutenga fedha kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madai pamoja na marejesho ya VAT; kutenga na kutoa fedha katika sekta za huduma za jamii (Priority Social Spending – PSS) ikiwemo sekta ya elimu, afya, barabara vijijini, makundi maalumu, kilimo, maji, umeme vijijini; pamoja na kuongeza ajira kwa watumishi kwa sekta za elimu na afya.

42. Mfumo wa bajeti wa mwaka 2023/24 unaonesha kuwa: Mapato ya ndani yameongezeka kwa wastani wa asilimia 12.0; mikopo ya kibiashara ya ndani na nje imepungua kwa asilimia 14.4; matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 10.4; matumizi ya maendeleo yameongezeka kwa wastani wa asilimia 1.0; bajeti kwa ajili ya malipo ya madeni yaliyohakikiwa yaimeongezeka kwa asilimia 129.6; bajeti ya miradi ya kielelezo (SGR na JNHPP) imeongezeka kwa asilimia 15.8; na bajeti ya miradi ambayo sio ya kimkakati/kielelezo imepungua kwa asilimia 11.9. Hivyo, asilimia 99.2 ya ongezeko la bajeti kwa mwaka 2023/24 imeelekezwa kwenye matumizi ya kawaida kutokana na kuongezeka kwa mishahara, malipo ya riba na gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali.

43. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 31,381.0, sawa na asilimia 70.7 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 13.0 hadi shilingi bilioni 26,725.4 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 23,652.8 mwaka 2022/23. Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 4,655.6 mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 4,365.1 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Ongezeko hili limezingatia maoteo ya ukuaji wa uchumi nchini unaotarajiwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo makusanyo halisi yalikua kwa asilimia 18.5 mwaka 2021/22 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2020/21 na asilimia 11.1 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ya kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwemo: Kuendelea kutambua na kusajili kampuni za kimataifa zinazoendesha biashara za kidigitali nchini kwa kutumia mfumo wa usajili

uliorahisishwa (simplified registration regime); kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inabadilishana taarifa; kuendelea na utaratibu wa kuingia makubaliano na walipakodi ili kuwawezesha kulipa madeni yao kwa awamu; kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka yote nchini kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo; kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vituo vya huduma kwa walipakodi na kampeni mbalimbali; kuendelea kusimamia mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Idara Zinazojitegemea; na kuwajengea uzalendo wananchi ili kujenga msingi wa ulipaji kodi kwa hiari.

44. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 5,466.2, sawa na asilimia 12.3 ya bajeti yote. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,440.4 kutoka soko la ndani ambapo shilingi bilioni 3,542.1 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi bilioni 1,898.3 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 2,100.5 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Katika Mafungu**

45. Katika mwaka 2023/24, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 29,232.1 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 12,771.5 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu na shilingi bilioni 10,882.1 kwa ajili ya mishahara ikiwemo upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya. Aidha, shilingi bilioni 6,396.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikijumuisha shilingi bilioni 200.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi na wazabuni.

46. Kufuatia maboresho katika sekta ya Afya na Elimu ambapo uwekezaji mkubwa umefanyika katika ujenzi wa miundombinu katika sekta hizo, bajeti ya mishahara imeongezeka kutoka shilingi bilioni 9,830.8 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 10,882.1 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Aidha, ongezeko hili linachangiwa na gharama za ajira mpya, upandishwaji vyeo kwa watumishi, malipo ya malimbikizo ya mishahara na mababiliko ya miundo kwa baadhi ya taasisi.

47. Riba kwa mikopo ya ndani imeongezeka kutoka shilingi bilioni 1,770.2 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 2,779.4 sawa na ongezeko la asilimia 58.1. Ongezeko hili linatokana na malipo ya riba ya NDF ya mwaka 2022/23. Vilevile, ongezeko hilo linasababishwa na kuongezeka kwa *yield* ambapo kwa mnada wa hatifungani ya miaka ishirini, *yield hiyo* imeongezeka kufikia asilimia 12.6 kwa mnada wa tarehe 16.2.2023 kutoka asilimia 11.6 kwa mnada wa tarehe 14.4.2022. Malipo ya riba za mikopo ya nje yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1,100.8 hadi shilingi bilioni 1,364.4 sawa na ongezeko la asilimia 23.9. Hii ni kutokana na kuendelea kupanda kwa riba za mikopo ya

kibiashara. Malipo ya mtaji kwa mikopo ya ndani (roll-over) inatarajiwa kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa madeni ya ndani yanayoiva mwaka 2023/24 ikijumuisha hatifungani maalumu ya Benki Kuu yenye kiasi cha shilingi bilioni 750 ambayo inaiva Juni 2024.

**Bajeti ya Maendeleo Katika Mafungu**

48. Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 15,156.0. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 11,873.9 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 78.3 ya bajeti ya maendeleo na shilingi bilioni 3,282.1 ni fedha za nje. Fedha za maendeleo za ndani zinajumuisha: shilingi bilioni 1,500.0 kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge*; shilingi bilioni 1,450.0 kwa ajili ya kugharamia mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; shilingi bilioni 1,310.1 kwa ajili ya Mfuko wa Barabara; shilingi bilioni 899.2 kwa ajili ya mifuko ya Reli, Maji na REA; shilingi bilioni 528.0 kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni yaliyohakikiwa ya makandarasi. Bajeti ya matumizi ya maendeleo ni sawa na asilimia 34.1 ya bajeti yote. Ukomo huu upo ndani ya wigo wa kati ya asilimia 30 na 40 ulioanishwa kwenye Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26). Utengaji huu wa fedha za maendeleo umezingatia ukamilishaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo inayoendelea. Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kufuatia kukamilika kwa miradi ya maendeleo hususan kwenye sekta za huduma za jamii ambazo kwa sasa zinahitaji fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya uendeshaji.

49. Viwango vinavyopendekezwa vya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma vinapatikana katika **Kiambatisho A1** na **Kiambatisho A2**.

50. Kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama ulivyoelezwa hapo juu, mfumo wa bajeti kwa mwaka 2023/24 ni kama unavyooneshwa katika **Jedwali Na. 8**.

### Jedwali Na. 8: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2023/24

| | | | | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mapato | 2022/23 | 2023/24 | Ongezeko/ Upungufu | Ongezeko /Upungufu (Asilimia) |
| A. | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | **27,005,581** | **30,237,128** | **3,231,547** | **12.0%** |
| | (i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi (TRA) | *23,652,758* | *26,725,409* | **3,072,651** | **13.0%** |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | *3,352,824* | *3,511,719* | **158,896** | **4.7%** |
| B. | **Mapato ya Halmashauri** | **1,012,286** | **1,143,883** | **131,597** | **13.0%** |
| C. | **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | **4,648,561** | **5,466,215** | **817,654** | **17.6%** |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | *1,949,480* | *2,184,134* | **234,654** | **12.0%** |
| | (ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | *2,576,958* | *3,151,958* | **575,000** | **22.3%** |
| | (iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | *122,123* | *130,123* | **8,000** | **6.6%** |
| D. | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **8,814,152** | **7,540,840** | **-1,273,311** | **-14.4%** |
| | (i) Mikopo ya Nje | *3,034,004* | *2,100,464* | **-933,540** | **-30.8%** |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | *2,480,148* | *1,898,316* | **-581,832** | **-23.5%** |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | *3,300,000* | *3,542,061* | **242,061** | **7.3%** |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | **41,480,580** | **44,388,067** | **2,907,487** | **7.0%** |
| | | | | | |
| | Matumizi | | | | |
| E. | **Matumizi ya Kawaida** | **26,474,578** | **29,232,092** | **2,757,514** | **10.4%** |
| | | | | | |
| | o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | **11,308,364** | **12,771,533** | **1,463,169** | **12.9%** |
| | -Malipo ya Riba Ndani | *1,770,159* | *2,799,374* | **1,029,215** | **58.1%** |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | *3,300,000* | *3,542,061* | **242,061** | **7.3%** |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | *2,916,041* | *2,763,947* | **-152,095** | **-5.2%** |
| | - Malipo ya Riba Nje | *1,100,802* | *1,364,377* | **263,575** | **23.9%** |
| | - Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | *1,655,652* | *1,710,608* | **54,955** | **3.3%** |
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | *565,710* | *591,167* | **25,457** | **4.5%** |
| | (ii) Mishahara | ***9,830,753*** | ***10,882,126*** | **1,051,373** | **10.7%** |
| | (iii)Matumizi Mengineyo (OC) | ***5,335,461*** | ***5,578,433*** | **242,972** | **4.6%** |
| | - Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *200,000* | *200,000* | **0** | **0.0%** |
| | - Matumizi ya Halmashauri (own source) | *617,485* | *749,083* | **131,597** | **21.3%** |
| | - Matumizi mengineyo | 4,517,976 | 4,629,351 | **111,375** | **2.5%** |
| F. | **Matumizi ya Maendeleo** | **15,006,002** | **15,155,975** | **149,973** | **1.0%** |
| | (i) Fedha za Ndani | *12,306,921* | *11,873,894* | **-433,027** | **-3.5%** |
| | o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *230,000* | *528,000* | **298,000** | **129.6%** |
| | o/w Ugharamiaji wa SGR | *1,113,000* | *1,500,000* | **387,000** | **34.8%** |
| | o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere | *1,435,000* | *1,450,000* | **15,000** | **1.0%** |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri (own Source) | *394,801* | *394,801* | **0** | **0.0%** |
| | o/w Miradi mingine | *9,134,120* | *8,001,093* | **-1,133,027** | **-12.4%** |
| | (ii) Fedha za Nje | *2,699,081* | *3,282,081* | **583,000** | **21.6%** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | **41,480,580** | **44,388,067** | **2,907,487** | **7.0%** |
| | **NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)** | **3.3%** | **2.7%** | | |

***Chanzo***:*Wizara ya Fedha na Mipango*

**Tanbihi**: Fedha za maendeleo zinajumuisha fedha zinazopelekwa katika utekelezaji wa programu ya elimumsingi bila ada (current grant transfers to LGAs) na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu (current grant transfers to HESLB).

## V. HITIMISHO

51. Taarifa hii imetoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti katika kipindi miezi saba (Julai 2022 – Januari 2023); mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto za utekelezaji wa bajeti zilizojitokeza; mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo; na mapendekezo ya mfumo wa bajeti kwa mwaka 2023/24.

52. Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Mwaka 2023/24 yatakuwa ni ya tatu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Maeneo ya vipaumbele yatakayozingatiwa ni kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24.

53. Katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ili kugharamia sehemu kubwa ya matumizi yake na kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na sheria nyingine kwa lengo la kubana matumizi na kuelekeza fedha kwenye utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa.

## KIAMBATISHO A1

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2022/23 | Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24 | Ongezeko / Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| | **MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni)** | | | |
| | **MFUKO MKUU WA SERIKALI** | | | |
| 001 | Deni la Serikali | 9,093,985 | 10,469,759 | 15.1% |
| 022 | Consolidated Fund Service | 2,214,380 | 2,301,774 | 3.9% |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **11,308,364** | **12,771,533** | **12.9%** |
| | **WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI** | | | |
| 002 | Tume ya Utumishi wa Walimu | 6,708 | 7,714 | 15.0% |
| 003 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | 1,480 | 2,294 | 55.0% |
| 004 | Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,500 | 1,575 | 5.0% |
| 005 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 63,174 | 66,333 | 5.0% |
| 006 | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | 5,147 | 6,905 | 34.1% |
| 007 | Msajili wa Hazina | 37,230 | 37,591 | 1.0% |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 2,048 | 2,651 | 29.4% |
| 012 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 2,700 | 4,861 | 80.0% |
| 013 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 2,916 | 3,861 | 32.4% |
| 014 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 23,180 | 25,111 | 8.3% |
| 015 | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 1,920 | 2,516 | 31.0% |
| 016 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 6,943 | 9,290 | 33.8% |
| 018 | Tume ya Elimu na Sayansi | 1,532 | 1,609 | 5.0% |
| 019 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 9,473 | 11,947 | 26.1% |
| 020 | IKULU | 21,709 | 24,039 | 10.7% |
| 021 | Hazina | 1,181,695 | 986,139 | -16.5% |
| 023 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 39,552 | 41,529 | 5.0% |
| 024 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania | 7,929 | 8,325 | 5.0% |
| 025 | Waziri Mkuu (Ofisi Binafsi) | 14,000 | 15,734 | 12.4% |
| 026 | Makamu wa Rais (Ofisi Binafsi) | 12,000 | 13,480 | 12.3% |
| 027 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 20,080 | 22,584 | 12.5% |
| 028 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Jeshi la Polisi | 296,515 | 316,394 | 6.7% |
| 029 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Magereza | 99,254 | 106,240 | 7.0% |
| 030 | Ofisi ya Rais na Baraza la Mawaziri | 570,805 | 617,463 | 8.2% |
| 031 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 10,520 | 12,098 | 15.0% |
| 032 | Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora | 18,084 | 19,988 | 10.5% |
| 033 | Sekretarieti ya Maadili | 6,543 | 7,870 | 20.3% |
| 034 | Wizara ya Mammbo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 188,937 | 213,423 | 13.0% |
| 035 | Ofisi ya Mwendesha Mashataka wa Serikali | 22,069 | 28,172 | 27.7% |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*

**Tanbihi**: Bajeti ya Fungu 021 kwa mwaka 2023/24 imepungua ikilinganishwa na mwaka 2022/23 kutokana na kutolewa kwa matumizi ya mara moja yaliyokuwa yametengwa katika bajeti ya mwaka 2022/23 ikiwemo ruzuku ya mafuta.

## KIAMBATISHO A1 inaendelea ...

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2022/23** | **Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24** | **Ongezeko / Upungufu** |
| 037 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 15,310 | 17,975 | 17.4% |
| 038 | Wizara ya Ulinzi (Ng'ome) | 400,416 | 425,207 | 6.2% |
| 039 | Jeshi la Kujenga Taifa | 135,769 | 145,773 | 7.4% |
| 040 | Mfuko wa Mahakama | 57,774 | 69,620 | 20.5% |
| 041 | Wizara ya Katiba na Sheria | 6,865 | 8,209 | 19.6% |
| 042 | Mfuko wa Bunge | 103,670 | 108,854 | 5.0% |
| 043 | Wizara ya Kilimo | 50,252 | 52,765 | 5.0% |
| 044 | Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji | 8,729 | 11,165 | 27.9% |
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 59,839 | 65,831 | 10.0% |
| 046 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 33,260 | 34,923 | 5.0% |
| 048 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 33,919 | 37,615 | 10.9% |
| 049 | Wizara ya Maji | 16,701 | 18,036 | 8.0% |
| 050 | Wizara ya Fedha na Mipango | 35,511 | 51,740 | 45.7% |
| 051 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 16,496 | 18,094 | 9.7% |
| 052 | Wizara ya Afya | 222,723 | 140,409 | -37.0% |
| 053 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 18,169 | 25,078 | 38.0% |
| 055 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 4,099 | 5,304 | 29.4% |
| 056 | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 15,138 | 30,895 | 104.1% |
| 057 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 13,660 | 15,343 | 12.3% |
| 058 | Wizara ya Nishati | 68,226 | 71,637 | 5.0% |
| 059 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 2,424 | 4,245 | 75.1% |
| 061 | Tume ya Uchaguzi | 4,970 | 5,719 | 15.1% |
| 062 | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Uchukuzi | 27,071 | 28,424 | 5.0% |
| 064 | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Uvuvi | 27,803 | 32,693 | 17.6% |
| 065 | Ofisi Ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu | 7,085 | 9,139 | 29.0% |
| 067 | Sekretarieti ya Ajira | 3,232 | 5,393 | 66.9% |
| 068 | Wizara ya Habari, Mawasiliano na ya Habari | 9,030 | 10,482 | 16.1% |
| 069 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 267,822 | 290,213 | 8.4% |
| 091 | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya | 9,847 | 12,340 | 25.3% |
| 092 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania | 1,213 | 1,773 | 46.2% |
| 093 | Idara Kuu ya Uhamiaji | 35,805 | 39,197 | 9.5% |
| 094 | Tume ya Utumishi wa Umma | 3,379 | 5,751 | 70.2% |
| 096 | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | 11,393 | 12,963 | 13.8% |
| 098 | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Ujenzi | 3,654 | 4,437 | 21.4% |
| 099 | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Mifugo | 23,984 | 25,183 | 5.0% |
| 100 | Wizara ya Madini | 40,836 | 45,877 | 12.3% |
| | **Jumla ndogo (B)** | **4,471,715** | **4,506,038** | **0.8%** |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*

**Tanbihi**: Bajeti ya Fungu 052 kwa mwaka 2023/24 imepungua ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa mwaka 2022/23 kutokana na kuondolewa kwa bajeti ya matumizi yenye vyanzo vya makusanyo ya Hospitali za Rufaa za Mikoa.

## KIAMBATISHO A1 inaendelea ...

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti iliyoidhinishwa (Matumizi Mengineyo - OC) 2022/23** | **Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24** | **Ongezeko / Upungufu** |
| | **SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** | | | |
| 036 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 2,166 | 2,876 | 32.8% |
| 047 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 2,437 | 3,161 | 29.7% |
| 054 | Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe | 2,069 | 2,775 | 34.1% |
| 063 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 2,659 | 3,394 | 27.7% |
| 070 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 3,307 | 4,225 | 27.7% |
| 071 | Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani | 3,643 | 4,428 | 21.5% |
| 072 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 3,802 | 4,594 | 20.8% |
| 073 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | 2,820 | 3,563 | 26.4% |
| 074 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | 3,309 | 4,427 | 33.8% |
| 075 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 2,850 | 3,595 | 26.1% |
| 076 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | 2,788 | 3,680 | 32.0% |
| 077 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | 3,352 | 4,622 | 37.9% |
| 078 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | 3,071 | 3,827 | 24.6% |
| 079 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | 4,243 | 5,058 | 19.2% |
| 080 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 3,042 | 3,997 | 31.4% |
| 081 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 3,116 | 4,024 | 29.1% |
| 082 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | 3,502 | 4,279 | 22.2% |
| 083 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | 2,456 | 3,181 | 29.5% |
| 084 | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | 2,764 | 3,504 | 26.8% |
| 085 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 4,187 | 4,998 | 19.4% |
| 086 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 3,787 | 4,578 | 20.9% |
| 087 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 3,549 | 4,529 | 27.6% |
| 088 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam | 2,476 | 3,352 | 35.4% |
| 089 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 2,531 | 3,260 | 28.8% |
| 090 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | 2,428 | 3,152 | 29.8% |
| 095 | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 2,745 | 3,985 | 45.2% |
| | **Jumla Ndogo (C )** | **79,099** | **101,066** | **27.8%** |
| | **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | |
| | ikiwemo Kilimo | 6,945 | 9,580 | 37.9% |
| | Afya | 27,032 | 32,032 | 18.5% |
| | Ujenzi | 4,573 | 5,891 | 28.8% |
| | Elimu Msingi | 46,879 | 53,468 | 14.1% |
| | Elimu Sekondari | 26,980 | 31,521 | 16.8% |
| | Utawala | 54,751 | 60,292 | 10.1% |
| | Stahili za Viongozi | - | 19,820 | |
| | Uhamisho na likizo kwa watumishi wasio walimu | - | 9,642 | |
| | **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | 617,485 | 749,083 | 21.3% |
| | **Jumla Ndogo ( D)** | **784,646** | **971,329** | 23.8% |
| | **Mishahari (E)** | 9,830,753 | 10,882,126 | 10.7% |
| | **Jumla Kuu Matumizi ya Kawaida (A+B+C+D+E)** | **26,474,578** | **29,232,092** | **10.4%** |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*

# KIAMBATISHO A2

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (FEDHA ZA NDANI NA NJE) KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23** | | | **Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24** | | | **Ongezeko / Upungufu** |
| | **WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA NA TAASISI ZA SERIKALI** | **Ndani** | **Nje** | **Jumla** | **Ndani** | **Nje** | **Jumla** | |
| 002 | Tume ya Utumishi wa Walimu | 670 | - | 670 | 670 | - | 670 | 0.0% |
| 003 | Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi | 1,410 | - | 1,410 | 1,410 | - | 1,410 | 0.0% |
| 004 | Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,410 | - | 1,410 | 450 | - | 450 | -68.1% |
| 005 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 288,464 | 11,500 | 299,964 | 250,000 | 3,405 | 253,405 | -15.5% |
| 006 | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | - | - | - | 360 | - | 360 | |
| 007 | Msajili wa Hazina | 940 | 650 | 1,590 | 940 | - | 940 | -40.9% |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 012 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 013 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 470 | 470 | - | 455 | 455 | -3.2% |
| 014 | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 9,930 | - | 9,930 | 9,930 | - | 9,930 | 0.0% |
| 015 | Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 1,000 | - | 1,000 | 700 | - | 700 | -30.0% |
| 016 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 4,000 | 500 | 4,500 | 2,000 | 455 | 2,455 | -45.4% |
| 018 | Tume ya Elimu na Sayansi | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 019 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 020 | IKULU | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 021 | HAZINA | 1,257,970 | 29,785 | 1,287,755 | 1,146,191 | 115,581 | 1,261,772 | -2.0% |
| 023 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 1,880 | 965 | 2,845 | 1,880 | - | 1,880 | -33.9% |
| 024 | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania | 1,100 | - | 1,100 | 1,000 | 1,173 | 2,173 | 97.5% |
| 025 | Waziri Mkuu (Ofisi Binafsi) | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 026 | Makamu wa Rais (Ofisi Binafsi) | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 027 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 940 | - | 940 | 940 | - | 940 | 0.0% |
| 028 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Jeshi la Polisi | 32,000 | 500 | 32,500 | 27,093 | - | 27,093 | -16.6% |
| 029 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Magereza | 21,370 | - | 21,370 | 16,370 | - | 16,370 | -23.4% |
| 030 | Ofisi ya Rais na Baraza la Mawaziri | 62,698 | 101,395 | 164,093 | 62,698 | 2,010 | 64,708 | -60.6% |
| 031 | Ofisi ya Makamu wa Rais | 3,602 | 18,360 | 21,962 | 3,602 | 22,029 | 25,631 | 16.7% |
| 032 | Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora | 8,070 | - | 8,070 | 8,070 | 117 | 8,187 | 1.5% |
| 033 | Sekretarieti ya Maadili | 2,820 | 650 | 3,470 | 1,500 | 450 | 1,950 | -43.8% |
| 034 | Wizara ya Mammbo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 4,700 | - | 4,700 | 2,700 | 188 | 2,888 | -38.6% |
| 035 | Ofisi ya Mwendesha Mashataka wa Serikali | 8,000 | 630 | 8,630 | 6,000 | 860 | 6,860 | -20.5% |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*

## KIAMBATISHO A2 inaendelea....

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (FEDHA ZA NDANI NA NJE) KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23** | | | **Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24** | | | **Ongezeko / Upungufu** |
| 037 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 1,880 | 4,109 | 5,989 | 1,880 | 2,191 | 4,071 | -32.0% |
| 038 | Wizara ya Ulinzi (Ng'ome) | 56,368 | - | 56,368 | 48,868 | - | 48,868 | -13.3% |
| 039 | Jeshi la Kujenga Taifa | 13,966 | - | 13,966 | 13,966 | - | 13,966 | 0.0% |
| 040 | Mfuko wa Mahakama | 36,002 | 3,091 | 39,093 | 31,002 | 53,777 | 84,779 | 116.9% |
| 041 | Wizara ya Katiba na Sheria | 5,111 | 7,616 | 12,727 | 5,111 | 10,451 | 15,562 | 22.3% |
| 042 | Mfuko wa Bunge | 4,700 | 700 | 5,400 | 4,700 | 469 | 5,169 | -4.3% |
| 043 | Wizara ya Kilimo | 185,979 | 82,927 | 268,906 | 185,979 | 58,913 | 244,891 | -8.9% |
| 044 | Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji | 30,347 | 450 | 30,797 | 30,347 | 13,600 | 43,947 | 42.7% |
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 7,828 | 3,099 | 10,927 | 7,828 | 584 | 8,412 | -23.0% |
| 046 | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 778,084 | 181,464 | 959,547 | 778,084 | 108,789 | 886,873 | -7.6% |
| 048 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 14,006 | 13,147 | 27,153 | 14,006 | 28,572 | 42,578 | 56.8% |
| 049 | Wizara ya Maji | 407,065 | 250,834 | 657,899 | 407,065 | 205,646 | 612,711 | -6.9% |
| 050 | Wizara ya Fedha na Mipango | 22,118 | 4,641 | 26,759 | 21,758 | 61,335 | 83,094 | 210.5% |
| 051 | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi | 57,600 | 6,778 | 64,378 | 37,600 | 4,695 | 42,295 | -34.3% |
| 052 | Wizara ya Afya | 410,298 | 144,834 | 555,132 | 410,298 | 310,976 | 721,274 | 29.9% |
| 053 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 6,900 | 4,192 | 11,092 | 4,300 | 1,102 | 5,402 | -51.3% |
| 055 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | - | 115 | 115 | - | - | - | -100.0% |
| 056 | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 758,726 | 124,313 | 883,039 | 758,726 | 324,370 | 1,083,096 | 22.7% |
| 057 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 160,000 | - | 160,000 | 160,000 | - | 160,000 | 0.0% |
| 058 | Wizara ya Nishati | 2,655,556 | 167,473 | 2,823,030 | 2,609,156 | 487,080 | 3,096,236 | 9.7% |
| 059 | Tume ya Kurekebisha Sheria | - | - | - | - | - | - | 0.0% |
| 061 | Tume ya Uchaguzi | 940 | - | 940 | 940 | 188 | 1,128 | 20.0% |
| 062 | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Uchukuzi | 1,927,772 | 113,463 | 2,041,235 | 1,861,065 | 107,265 | 1,968,330 | -3.6% |
| 064 | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Uvuvi | 98,682 | 36,997 | 135,679 | 98,682 | 23,730 | 122,412 | -9.8% |
| 065 | Ofisi Ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu | 13,000 | 13,656 | 26,656 | 13,000 | 936 | 13,936 | -47.7% |
| 067 | Sekretarieti ya Ajira | 3,658 | - | 3,658 | 3,573 | - | 3,573 | -2.3% |
| 068 | Wizara ya Habari, Mawasiliano na ya Habari | 215,777 | 40,000 | 255,777 | 146,777 | 35,177 | 181,954 | -28.9% |
| 069 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 109,880 | 70,557 | 180,436 | 109,880 | 58,287 | 168,167 | -6.8% |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*

## KIAMBATISHO A2 inaendelea....

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (FEDHA ZA NDANI NA NJE) KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23 | | | Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24 | | | Ongezeko / Upungufu |
| 091 | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya | - | - | - | 2,000 | 6,775 | 8,775 | |
| 092 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania | 1,880 | 10,122 | 12,002 | 1,880 | 20,312 | 22,192 | 84.9% |
| 093 | Idara Kuu ya Uhamiaji | 12,235 | - | 12,235 | 8,241 | - | 8,241 | -32.6% |
| 094 | Tume ya Utumishi wa Umma | 300 | - | 300 | 300 | - | 300 | 0.0% |
| 096 | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | 15,831 | - | 15,831 | 10,831 | - | 10,831 | -31.6% |
| 098 | Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Ujenzi | 1,124,576 | 252,966 | 1,377,542 | 1,084,666 | 229,110 | 1,313,777 | -4.6% |
| 099 | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi - Mifugo | 46,592 | 139 | 46,731 | 46,592 | 5,332 | 51,924 | 11.1% |
| 100 | Wizara ya Madini | 22,000 | - | 22,000 | 22,000 | 1,173 | 23,173 | 5.3% |
| | **Jumla Ndogo(A)** | **10,918,630** | **1,703,088** | **12,621,718** | **10,485,603** | **2,307,555** | **12,793,158** | **1.4%** |

***Chanzo***:*Wizara ya Fedha na Mipango*

| MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA WIZARA, IDARA ZINAZOJITEGEMEA, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (FEDHA ZA NDANI NA NJE) KWA MWAKA 2023/24 (Shilingi Milioni) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fungu** | **Jina la Fungu** | **Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23** | | | **Mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2023/24** | | | **Ongezeko / Upungufu** |
| | **SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** | **Ndani** | **Nje** | **Jumla** | **Ndani** | **Nje** | **Jumla** | |
| 036 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 1,901 | 413 | 2,314 | 1,901 | 682 | 2,583 | 11.6% |
| 047 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 2,359 | 550 | 2,909 | 2,359 | 603 | 2,962 | 1.8% |
| 054 | Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe | 2,372 | 545 | 2,917 | 2,372 | 956 | 3,327 | 14.1% |
| 063 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 2,242 | 570 | 2,812 | 2,242 | 12,130 | 14,371 | 411.0% |
| 070 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 1,273 | 430 | 1,703 | 1,273 | 8,713 | 9,985 | 486.5% |
| 071 | Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani | 2,860 | 502 | 3,362 | 2,860 | 691 | 3,551 | 5.6% |
| 072 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 1,270 | 610 | 1,880 | 1,270 | 687 | 1,956 | 4.1% |
| 073 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | 1,257 | 833 | 2,090 | 1,257 | 10,198 | 11,456 | 448.0% |
| 074 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | 2,461 | 754 | 3,214 | 2,461 | 7,747 | 10,208 | 217.6% |
| 075 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 3,316 | 436 | 3,751 | 3,316 | 616 | 3,931 | 4.8% |
| 076 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | 1,923 | 3,986 | 5,909 | 1,923 | 8,008 | 9,931 | 68.1% |
| 077 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mara | 2,573 | 644 | 3,217 | 2,573 | 668 | 3,241 | 0.8% |
| 078 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | 2,027 | 985 | 3,012 | 2,027 | 954 | 2,981 | -1.0% |
| 079 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | 3,363 | 431 | 3,794 | 3,363 | 947 | 4,309 | 13.6% |
| 080 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 1,752 | 582 | 2,334 | 1,752 | 962 | 2,715 | 16.3% |
| 081 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 1,568 | 597 | 2,165 | 1,568 | 721 | 2,289 | 5.7% |
| 082 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | 1,700 | 586 | 2,286 | 1,700 | 645 | 2,345 | 2.6% |
| 083 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | 2,252 | 554 | 2,806 | 2,252 | 925 | 3,178 | 13.2% |
| 084 | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | 3,214 | 563 | 3,777 | 3,214 | 873 | 4,087 | 8.2% |
| 085 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 2,343 | 549 | 2,893 | 2,343 | 579 | 2,923 | 1.0% |
| 086 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 2,128 | 552 | 2,680 | 2,128 | 962 | 3,090 | 15.3% |
| 087 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 2,044 | 626 | 2,670 | 2,044 | 724 | 2,768 | 3.7% |
| 088 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam | 11,291 | 482 | 11,772 | 11,291 | 744 | 12,035 | 2.2% |
| 089 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 1,874 | 399 | 2,272 | 1,874 | 522 | 2,396 | 5.4% |
| 090 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | 2,224 | 784 | 3,008 | 2,224 | 893 | 3,116 | 3.6% |
| 095 | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 2,434 | 546 | 2,980 | 2,434 | 632 | 3,066 | 2.9% |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **66,019** | **18,508** | **84,527** | **66,019** | **62,781** | **128,799** | **52.4%** |
| | | | | | | | | |
| | **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | | | | |
| | **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | 927,471 | 977,485 | 1,904,956 | 927,471 | 911,745 | 1,839,216 | -3.5% |
| | **Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa** | 394,801 | | 394,801 | 394,801 | - | 394,801 | 0.0% |
| | **Jumla Ndogo ( C)** | **1,322,272** | **977,485** | **2,299,757** | **1,322,272** | **911,745** | **2,234,017** | -2.9% |
| | | | | | | | | |
| | **Jumla Kuu Matumizi ya Maendeleo (A+B+C)** | **12,306,921** | **2,699,081** | **15,006,002** | **11,873,894** | **3,282,081** | **15,155,975** | **1.0%** |

***Chanzo**:Wizara ya Fedha na Mipango*